JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

Simu: 022-2121600
Faksi: 022-2113271 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Tz
Tovuti: www.moe.go.tz

NAFASI ZA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA CHETI NA STASHAHADA: JULAI 2010/2011

Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi anatangaza nafasi za mafunzo ya ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada kama ifuatavyo:

MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA CHETI (TARAJALI)

1. CHETI DARAJA LA IIIA: MUDA NI MIAKA 2

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

(a) Ufaulu wa kidato cha 4 (mwaka 2009) usiopungua alama 28 katika kikao kimoja.

(b) Ufaulu wa kidato cha 4 usiopungua 'credit' 4 kwa kiwango cha C au zaidi katika kikao kimoja au zaidi.

(c) Kuhitimu kidato cha 6 ni sifa ya nyongeza.

Kipaumbele kitatolewa kwa waliofaulu masomo ya Hisabati, Sayansi, 'English', na 'French'.

2. CHETI MAALUMU DARAJA LA IIIA (MICHEZO): MUDA NI MIAKA 2

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

(a) Ufaulu wa kidato cha 4 usiopungua alama 28.

(b) Kuhitimu kidato cha 6 ni sifa ya nyongeza.

(c) Mwelekeo katika michezo (vithibitisho ni muhimu).

Kipaumbele kitatolewa kwa waliofaulu masomo ya Hisabati, Sayansi, 'English', na 'French'.

MAFUNZO YA WALIMU KAZINI

1. CHETI DARAJA LA IIIA (SAYANSI KIMU): MUDA WA MAFUNZO NI MWAKA 1.

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

(a) Awe mwalimu kazini aliyepitia mafunzo ya Ualimu Daraja IIIA.

(b) Awe na uzoefu kazini usiopungua miaka 3.

(c) Awe alifaulu masomo ya Sayansi Kimu au Sayansi katika mtihani wa Kidato cha 4 kwa kiwango kisichopungua alama 28.

2. CHETI DARAJA LA IIIA (ELIMU MAALUM): MUDA WA MAFUNZO MWAKA 1.

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

(a) Awe mwalimu kazini aliyepitia mafunzo ya Ualimu Daraja IIIA.
(b) Awe amefundisha kwa muda usiopungua miaka 3.
(c) Awe alifaulu angalau somo moja la Sayansi katika mtihani wa Kidato cha Nne.
(d) Awe mwalimu anayefundisha Elimu Maalum bila mafunzo rasmi.

MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU

1. STASHAHADA YA UALIMU (TARAJALI) : MUDA WA MAFUNZO MIAKA 2.

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

(a) Ufaulu wa Kidato cha 6 kwa kiwango kisichopungua 'Principal Pass' moja na 'subsidiary' moja katika masomo
atakayofundisha shule za sekondari (Kidato cha 1 hadi 4). Masomo ya Economics na General Studies hayatahusika. AU
awe na cheti cha FTC na kufaulu katika masomo ya Sayansi na Hisabati.

(b) Ufaulu wa somo la English katika mtihani wa kumaliza Kidato cha 4 kwa kiwango cha A,B,C au D ni sifa ya nyongeza.

2. STASHAHADA YA UALIMU (KAZINI): MUDA WA MAFUNZO MIAKA 2.

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

(a) Awe mwalimu anayefundisha na mwenye Cheti cha Ualimu (IIIA) na uzoefu kazini usiopungua miaka mitatu.

(b) Awe amefaulu Kidato cha 6 kwa kiwango kisichopungua 'Principal Pass' moja na 'subsidiary' moja katika masomo
atakayofundisha shule za sekondari (Kidato cha 1 hadi 4). Masomo ya Economics na General Studies hayatahusika. .

3. STASHAHADA YA UALIMU (ELIMU MAALUM): MUDA WA MAFUNZO MIAKA 2.

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

(a) Awe mwalimu mwenye Cheti cha Ualimu Daraja la IIIA cha Elimu Maalumu na kufaulu masomo mawili Kidato cha Sita, AU

(b) Awe mwalimu mwenye Stashahada ya Ualimu fani ya Sayansi/Sayansi ya Jamii na awe na uzoefu kazini usiopungua
miaka 3.

(c) Awe amefaulu Kidato cha 6 kwa kiwango kisichopungua 'Principal Pass' moja na 'subsidiary' moja na anapenda kufundisha
watoto wenye mahitaji maalum (wasioona, viziwi, watoto wenye ulemavu wa akili).

4. STASHAHADA YA UALIMU (SAYANSI KIMU): MUDA WA MAFUNZO NI MIAKA 2.

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

(a) Awe mwalimu mwenye Cheti cha: Ualimu Daraja IIIA, Sayansi Kimu na kufaulu Kidato cha 6 kwa kiwango kisichopungua
"Principal Pass" moja na "Subsidiary" moja katika masomo ya: Baiyolojia, Kemia na Sayansi Kimu

AU

(b) Awe amefaulu kwa kiwango kisichopungua "Principal Pass" moja na "Subsidiary" moja katika mitihani Kidato cha 6 katika

masomo ya Sayansi Kimu na somo mojawapo kati ya: Baiyolojia, Kemia, Kilimo, Fizikia, Hisabati, 'Textile' na 'Nutrition'

5. MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU (MICHEZO, MUZIKI, SANAA MAONESHO/UFUNDI):
MUDA WA MAFUNZO NI MIAKA 2.
Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

(a) Awe mwalimu kazini aliyepitia mafunzo ya Ualimu Daraja IIIA na kujiendeleza hadi Kidato cha 6 na kufaulu kwa kiwango kisichopungua ''Principal Pass'' moja na "Subsidiary" moja kwa kuzingatia yafuatayo kwa kila kozi:

Sanaa za Maonesho: Ufaulu katika masomo ya English Literature, Kiswahili, Jiografia au Historia.

Muziki: Ufaulu katika masomo ya English, Kiswahili, Muziki, Historia, Jiografia na Fizikia.

Sanaa Ufundi: Ufaulu katika masomo ya "Fine Art" na /au masomo mengine yanayoendana na kozi yenyewe.

Elimu kwa Michezo: Ufaulu katika masomo ya Baiyolojia, Kemia, Fizikia, English na Kiswahili.

6. STASHAHADA YA UALIMU (UFUNDI): MUDA WA MAFUNZO MIAKA 2
Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

(a) Ufaulu katika mafunzo ya FTC kutoka vyuo vya Ufundi Arusha, Mbeya, Dar es Salaam au sifa zinazolingana.

7. STASHAHADA YA UALIMU (KILIMO): MUDA WA MAFUNZO NI MIAKA 2.
Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

(a) Ufaulu wa Kidato cha 6 kiwango cha angalau "Principal Pass" moja na "Subsidiary" moja katika masomo ya Bayologia na Kilimo au sifa zinazolingana.

8. STASHAHADA YA UALIMU (BIASHARA): MUDA WA MAFUNZO NI MIAKA 2.
Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

(a) Ufaulu wa Kidato cha 6 kwa kiwango kisichopungua 'Principal Pass' moja na 'Subsidiary' moja katika masomo ya Biashara na Uhasibu.

MAELEKEZO MUHIMU KWA WAOMBAJI WOTE

(i) Waombaji wa Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti (Daraja IIIA) watachaguliwa kupitia "Selforms" walizojaza wakati wanamaliza Kidato cha 4. Hata hivyo watapaswa kuthibitisha kwa kuwasilisha maombi kwa barua.

(ii) Waombaji wa mafunzo ya Stashahada wawe wamehitimu Kidato cha 6 kati ya mwaka 2005 na 2010 na wawe na ufaulu usiopungua 'Principal Pass' moja na 'Subsidiary' moja katika masomo yanayofundishwa Kidato cha I hadi 4

(iii) Maombi ya mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada yaambatanishwe na matokeo ya Kidato cha 4 na cha 6.

(iv) Maombi yaambatane na nakala za vyeti (Leaving and Academic Certificates) vya Kidato cha 4, 6, na Cheti cha Ualimu kwa wale ambao ni walimu tayari. Aidha, maombi yaambatane na picha mbili za mwombaji (passport size).

(v) Mwombaji aoneshe umri, jinsi (mwanamme / mwanamke) na umri kazini kwa wale walioajiriwa.

(vi) Upo uwezekano wa kupata mafunzo ya ualimu mwanachuo akiwa anaishi nje ya chuo. Endapo mwombaji atapenda kusoma akiwa nje ya chuo, aeleze na ataje chuo anachopendelea kusoma.
(vii) Barua za waombaji wa Mafunzo ya Walimu Kazini zipitishwe na waajiri wao.
(viii) Mafunzo yataanza Julai 2010.

KUAJIRIWA BAADA YA MAFUNZO

(i) Wahitimu wa Mafunzo ya Ualimu (tarajali) ngazi ya Cheti na Stashahada wana nafasi ya kuajiriwa serikalini.
(ii) Wahitimu wa Mafunzo ya Ualimu (Kazini) ngazi ya Stashahada Elimu Maalum, Sayansi Kimu, Sanaa, Ufundi, Maonesho,
Muziki na Michezo ambao ni waajiriwa watarudi kwa waajiri wao kufundisha fani walizosomea.

GHARAMA ZA MAFUNZO

Ada kwa Mafunzo ya Ualimu (tarajali) ngazi ya Cheti (Daraja A) na Stashahada (tarajali na mafunzo kazini) kwa kila mwaka wa masomo ni sh. 150,000/=.

USAILI

Waombaji wote watakaochaguliwa watafanyiwa usaili chuoni ikiwa ni pamoja na uhakiki wa uhalali wa vyeti kabla ya kujiunga na mafunzo ya Ualimu.

ANGALIZO

Tahadhari inatolewa kwa matumizi ya vyeti vya kughushi na udanganyifu wa aina yoyote. Watakaohusika na udanganyifu wowote watashughulikiwa kikamilifu ikiwa ni pamoja na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Kwa kuzingatia idadi ya waombaji wanaotarajiwa, majibu yatatolewa kwa watakaoteuliwa tu.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 3/5/2010. Tangazo hili lipo pia katika tovuti ya Wizara:www.moe.go.tz

Maombi yatumwe kwa:
KATIBU MKUU,
WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI,
S.L.P. 9121,
DAR ES SALAAM.

(Aione Mkurugenzi, Elimu ya Ualimu)